رِسَالَةٌ إِلَى مُحِبِّي آلِ البَيْتِ

UJUMBE

KWA

WAPENZI WA AHLUL BAIT

(Jamaa wa nyumba ya Mtume ﷺ)

1438 - 2017

رِسَالَةٌ إِلَى مُحِبِّي آلِ البَيْتِ

UJUMBE
KWA
WAPENZI WA AHLUL BAIT

(Jamaa wa nyumba ya Mtume ﷺ)

MTUNZI
KIKUNDI CHA WATAFITI
DAARUL-MUNTAQAA

بسم الله الرحمن الرحيم

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Kila sifa njema zinamsitahikia Allah, Mola wa walimwengu, na Sala na Salaamu zimfikie Mjumbe wake, ambae ni rehema kwa walimwengu, Nabii wetu na kiongozi wetu Muhammad ﷺ, na jamaa zake wema wenye kutoharika, na maswahaba zake, na kila mwenye kumfuata yeye Mtume ﷺ kwa wema na akafuata mwenendo wake mpaka siku ya kiama.

Ama baada ya hayo:

Huu ni ujumbe tunautanguliza kwa kila mwenye akili, anaetanguliza akili yake mbele ya matamanio yake, akatanguliza haki mbele ya ukereketwa, akatambua haki kwa haki na si kwa watu, na akatambua kuwa haki inastahiki zaidi kufuatwa kuliko chengine chochote.

Huu ni ujumbe ambao tumeutoa kwa anuani ya [Ujumbe kwa wapenzi wa jamaa wa Mtume (Aalil Bait)]

Na ujumbe huu umechukuliwa kutoka katika vitabu vya mashia vyenye kutegemewa, kwani mashia

ni kama makundi mengineyo ya watu, wapo miongoni mwao wenye akili ambao wanapenda kheri na ndio wanayoitafuta, na endapo atadhihirishiwa huwa anaikubali bi idhnillah, na wapo miongoni mwao wenye kutanguliza, ukereketwa na kufuata watu wengine, wakaacha kutumia akili zao, wakafuata matamanio yao, pasi na hoja kutoka kwa Allah.

Na matumaini yetu ni kwamba mwenye kusoma ujumbe huu, ataupokea kwa kifua kikunjufu na akili yenye kufunguka, na kuwa tayari kuifuata haki popote ilipo kwani haki ni kitu chenye thamaniwa.

Na sasa tuanze kuuweka ujumbe huu mbele ya wasomaji:

1- Ikiwa uhusiano kati ya Ahlul Bait na Maswahaba wa Mtume ﷺ na nyumba nyengine za Makuraishi, ni uhusiano wa chuki, husda na ugomvi, kama ilivyotajwa katika vitabu vya Mashia, basi kuna siri gani ya kuitana majina na kuozeshana kati ya Ahlul Bait na Makuraishi wengine miongoni mwa Maswahaba na waliokuja baada yao!? Na mfano wa hayo:

a. Kuitwa baadhi ya watoto na wajukuu wa Ally رضي الله عنه kwa majina ya Maswahaba, na hasa jina la Abubakri, Umari, Uthman na Twalha (رضي الله عنهم), na miongoni mwao Abubakari bin Ally, Abubakari

bin Hassan, wameuawa Karbalaa pamoja na Hussein[1] ﷺ, Abubakri Ibnil Hassan Al Muthanna Ibnil Hassan As Sibti ﷺ, Abubakri bin Musa Al Qaadhwim.

Agma kujiita kwa Kun-ya ya Abubakri ﷺ, miongoni mwa waliojiita hivyo ni Ally Zainul 'Aabidiin bin Husein As Shahid, na Ally Ar Ridhwaa bin Musa Al Kaadhwim.

b. Ama kujiita kwa jina la Umar ﷺ, ni jina waliloitwa wengi miongoni mwa Ahlul Bait, bali jina hilo liliendelea mpaka katika kizazi cha kumi na nane, katika kizazi cha wajukuu wawili (ﷺ), miongoni mwao ni:

Umar Al Atwraf bin Ally[2], Umar bin Hassan, aliuawa huko Karbalaa pamoja na Hussein[3] ﷺ, Umar bin Hussein As Shahid, Umar Al Ashraf bin Ally Zainul 'Aabidiin, Umar (As Shajariy) ibnu Ally Al Aswghar ibnu Umar Al Ashraf bin Zainul 'Aabidiin.

Ama jina la Uthman ﷺ, pia walikuwepo kwenye

---

1 Angalia kitabu: Al Irshaad (Uk: 186, na 248) cha Al Mufiid.

2 Angalia kitabu: Kashful Ghumma Fii Ma'rifatil Aimmah (J: 2, Uk: 66) cha Ali Al Irbiliy.

3 Angalia kitabu: Al Irshaad (Uk: 197) cha Al Mufiid.

nyumba ya Mtume ﷺ, wanaoitwa kwa jina hilo, miongoni mwao:

Uthman bin Ally bin Abi Twaalib, mama yake akiitwa Ummul Baniin Al Kullaabiyyah, aliuawa pamoja na ndugu yake ambae ni Husein katika mji wa Twaffi, pia alikuwepo Uthman bin Yahya bin Suleiman, katika kizazi cha Ally bin Husein رضي الله عنه.

Jina la Twalha kwa Ahlul Bayt ni: Twalha bin Hassan (Hassan mjukuu wa Mtume ﷺ), na mama yake ni Ummu Is-haaqa bint Twalha bin Ubaidullahi رضي الله عنه[1], Twalha bin Hassan Almuthallath bin Hassan Almuthanna bin Hassan (Hassan mjukuu wa Mtume ﷺ).

Kuitwa kwa jina la Aisha kwa Ahlul Bait, miongoni mwa walioitwa jina la Aisha katika kizazi cha Ally رضي الله عنه: Aisha bint Imam Jafar Sswaadiq, Aisha bint Musa Alkaadhwim, Aisha bint Ally Arridhwaa, Aisha bint Ally Alhaadiy, Aisha bint Muhammad bin Hassan bin Jafar bin Hassani Almuthannaa.

Hivi hawakuwa Ahlul Bait ndio muongozo kwa Mashia katika kila kitu? Basi je wafuasi wao wanawafuata katika kuwaita kwa majina hayo watoto wao

[1] Angalia kitabu: Al Irshaad (Uk: 194) cha Al Mufiid.

wakiume na wakike? Hivi kuna Shia anayeweza kufanya ushujaa kwa kumuita mtoto wake Abubakri, Umar au Uthmani, au kumita mtoto bint yake kwa jina la Aisha??

c- Udugu uliozalikana kutokana na ndoa na nasaba kati ya Ahlul Bait Maswahaba, hasa hasa jamaa wa Abubakri, jamaa wa Al khatwaabi na watu wa Zubeir, ni jambo linalopatikana kwa wingi sana. Vitabu vya Mashia vyenye kutegemewa vinaelezea jambo hilo, miongoni mwake:

d- Kuolewa Ummu Kulthuum bint Ally رضي الله عنه na Umari bin Al khatwaab رضي الله عنه.

Hakika kuozesha Ally رضي الله عنه binti yake kwa Umari رضي الله عنه, si kwamba inajulisha juu ya ukubwa wa mafungamano na ukubwa wa mapenzi kati ya pande mbili tu, bali inajulisha ya kwamba Ally رضي الله عنه anamuona Umar ibnil Al khatwaabi kuwa ni mtu bora anastahiki kuwa mume wa mjukuu wa Mtume ﷺ, na hii ni kinyume na itikadi ya Mashia kwa Umar رضي الله عنه, na zingatia tamko lake Allah Mtukufu:

﴿وَٱلطَّيِّبَٰتُ لِلطَّيِّبِينَ وَٱلطَّيِّبُونَ لِلطَّيِّبَٰتِۚ أُوْلَٰٓئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَۖ لَهُم مَّغۡفِرَةٞ وَرِزۡقٞ كَرِيمٞ﴾

"Na wanawake wema ni kwa ajili ya wanaume wema, na wanaume wema ni kwa ajili ya wanawake wema.

Hao wameepushwa na hayo wanayo yasema; watapata msamaha na riziki njema "[1].

e- Fatma bint Ally bin Abi Twalib رضي الله عنهما aliolewa na Mundhir bin Ubaida bin Zubeir رضي الله عنهما.

f- Sakina bint Husein As Shahiid, aliolewa na Mus-abu bin Zubairi.

g- Ruqayyah bint Al Hassan رضي الله عنهما aliolewa na Amru bin zubeir رضي الله عنهما.

h- Fatma bint Husein As Shahiid aliolewa na Abdullahi ibn Amru ibn Uthman ibn Affaan رضي الله عنهما

i- Ummul Hassan bint Al Hasan (mjukuu wa Mtume ﷺ), aliolewa na Abdullahi bin Zubeir رضي الله عنهما.

j- Maliika bin Al Hasan [Almuthanna] aliolewa na Jafar bin Mus-abu bin Zubeir.

k- Alhassan bin Ally alimuoa Hafswa bint Abdur Rahmaan bin Abibakri رضي الله عنهما.

l- Al Hassan bin Ally رضي الله عنهما, alimuoa Ummu Is-haaqa bint Twalha bin Ubaidullah رضي الله عنهما, kisha kabla ya kufa Hassan رضي الله عنهما alimuusia ndugu yake Husein رضي الله عنهما As Shahiid amuoe baada yake, Husein رضي الله عنهما akamuoa na akamzali mtoto anyeitwa Fatma.

---

[1] Surat An Nuur/26.

m- Muhammad Al Baaqir alimuoa Ummu Farwa bint Qasim bin Muhammad bin Abibakri رضي الله عنهم[1] akamzalia mtoto ambaye ni Imam Jafar As Swaadiq.

2- Tunaona Mashia namna wanavyoji kurubisha kwa Allah kwa kuwatukana Maswahaba wakubwa, wa mwanzo ni Makhalifa watatu waongofu: Abubakri, Umar na Uthman رضي الله عنهم, lakini humpati Suni hata mmoja anayemtukana mmoja miongoni mwa Ahlul Bait! bali (Masuni) wanaji kurubisha kwa Allah kwa kuwapenda Ahlul Bait, na hili Mashia hawawezi kulipinga, hata kwa kutumia uwongo.

3- Vinaeleza vitabu vya Mashia kwamba Mtume ﷺ amewaeleza watu wa nyumba yake (Ahlul Bait) yale ambayo watu watazusha katika kuwachukia wao, kwa sababu Allah amempa habari kwa yale yatakayo tokea baada yake mpaka siku ya kiama, lakini Mashia katika vitabu vyao vyenye kutegemewa wanatoa hoja juu ya kuritadi kwa Maswahaba kwa hadithi ya

---

[1] Mafungamano ya kuozeshana baina ya watu wa Ali ﷺ na watoto wa Ami zao miongoni mwa watu wa Abubakri, watu wa Khatwaab, watu wa Uthman watu wa Zubeir hakika ni mafungamano makubwa mno, amedhibiti kwa idadi sheikh (Sayyid ibn Ahmad ibn Ibrahim, katika kitabu chake: Al Asmaa wal Muswaaharaat baina Ahlil Bait was Swahaaba îøõ úÓ ìÌÓÍ). Kwa mwenye kutaka ziada arejee kwenye kitabu hicho, kwani ni kitabu kizuri na kimekusanya mambo yanahusu mlango huu.

Haudhi: "Hakika wewe hujui yale waliyo yazusha baada yako, kwani hawakuacha kuwa ni wenye kurudi nyuma kwa visigino vyao (kuritadi)" [1].

Je haikuwa hadithi hii ni dalili ya kwamba Mtume ﷺ hajui yatayokuja baaada yake? Na ikiwa Mtume ﷺ hajui ghaibu (mambo yaliyo fichika) basi kwa mtu mwenginewe itakua ndio zaidi hajui.

4- Kitu gani ambacho amenufaika nacho Abubakri na Umar رضي الله عنهما kwa kutawalia kwao Ukhalifa (watawala), hawakujenga nyumba za fahari (Palace), hawakuacha Mali (kwa warithi wao), na wala hawakufanya uongozi uwe kwa watoto wao, bali Umar رضي الله عنه kuhusu jambo la ukhalifa aliliacha kwenye Shura ya watu sita, na akausia asiteuliwe ukhalifa yeyote katika watu wa familia ya Al Khatwaab.

5- Hakika Umar رضي الله عنه alichagua watu sita wakae Shura baada kufa kwake, watatu miongoni mwao wakajitoa, na Abdur Rahman ibn 'Auf nae akajitoa, akabakia Uthman na Ali رضي الله عنهما, kwa nini Ali رضي الله عنه tangu mwanzo hakusema kwamba yeye ndiye aliyeusiwa ukhalifa (kuwa mtawala baada ya Mtume ﷺ), je kuna yeyote aliye kuwa anamuogopa baada ya kufa Umar?!

---

[1] Muttafaqun Alayhi. Na amepokea Al Majlis katika: Bihaarul Anwaar: (J. 7, Uk. 27), na (J. 23, Uk. 165), na (J. 27, Uk. 27) na sehemu nyengine.

6- Mashia hawawezi kupinga kwamba Abubakri na Umar walimpa bai'a (kiapo cha utiifu) Mtume ﷺ chini ya mti, na kwamba Allah ameelezea kuwa yeye amewaridhia wao na aliyajua yaliyopo ndani ya mioyo yao, akasema:

﴿لَّقَدْ رَضِيَ ٱللَّهُ عَنِ ٱلْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ ٱلشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِى قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ ٱلسَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَٰبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا﴾

"Kwa hakika Allah amewaridhia waumini, pale walipokupa wewe Bai'a chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, basi akawalipa kwa (kuwapa) Ushindi wa karibu"[1].

Basi inawezekana vipi kwa Mashia hivi sasa kuipinga habari hii ya Allah na kuleta madai yaliyo kinyume na habari hii?! Kama vile wanataka kusema: "Ewe Mola hujui kwao (Maswahaba), yale tunayojua sisi"!.

7- Swala ni nguzo kubwa miongoni mwa nguzo za ki-matendo, basi vipi Mtume ﷺ amruhusu Abubakri رضي الله عنه kukaimu (kukaa badala yake) katika kuswalisha wakati yeye alipokuwa mgonjwa, na hali ya kuwa Ally رضي الله عنه yupo? Kwa nini Mtume ﷺ alimtanguliza Abubakri رضي الله عنه kuswalisha na hakumtanguliza Ally ambaye ni

[1] Surat Al fath/18.

wasii wake na Khalifa baada yake kama wanavyoitakidi Shia? Na ikiwa Abubakri amejitanguliza mbele yeye mwenyewe (pasi na kuteuliwa) kwa nini Ally ﷺ hakulipinga hilo na kumuamrisha arudi nyuma, ili yeye aswalishe sehemu yake, na kumtolea hoja juu yake kwamba yeye ndiye Khalifa wa Mtume ﷺ na ndiye wasii wake baada ya kufa kwake?

8- Baada ya kufa Mtume ﷺ alitawalia Ukhalifa (uongozi) Abubakri, kisha Umari, kisha Uthmani ﷺ, na Mashia wanawafanya hao kuwa ni Wapotevu, Madhalimu na ni Makafiri, wamewapora Ahlul Bait haki yao, basi je Ally, Ammaari, Salmaani na Miqdaadi ﷺ waliswali nyuma ya (makhalifa) hao au hapana? Na je kwa upande wa Mashia kuswali nyuma ya fasiki (muovu) swala inasihi?, sikwambii nyuma ya Naaswib na Kafiri?!

9- Ilikuwa kufunguliwa kwa miji ya (ya makafiri) kuwa chini ya Dola ya kiislamu katika zama za Abubakri, Umari, na Uthmani ﷺ ni ufunguzi mkubwa sana, miongoni mwake ni ufunguzi wa miji ya Fursi (Iran), Sham (Syria), Baitil Maqdis, Misri, Afrika na miji ya Sindi (Indus) na miji mingine, je jambo hilo linahesabiwa ni ushindi kutoka Allah kwa kuunusuru Uislamu au hapana? Na je yule ambaye akifanya kazi hizi wakati wa utawala (ukhalifa) wake

atazingatiwa kuwa ni mtawala Muovu na Dhalimu? Na lilikuaje jeshi ambalo lipo chini ya uongozi wake? Hakuna shaka kwamba lilikuwa kama alivyo kuwa kiongozi wao, hakika hao ni askari wenye kushambulia (vitani) na kulinda (katika miji yao), na wala hawasahau Mashia kwamba miongoni mwa askari hao waliofungua miji ni (Ally, Hassan, Husein, Salmaan, Abu Dharri na Ammaar رضي الله عنهم), basi ni ipi hukumu ya watu hawa bora???

10- Vitabu vya Mashia vyenye kutegemewa vimeafikiana (kuandika) kwamba uhusiano baina ya Umar na Ally رضي الله عنهما ulikuwa ni wa chuki na uadui, kisha tunapata kuwa Umari رضي الله عنه alimpa uamiri Ally رضي الله عنه kwa niaba yake kwenye vita kwenda kuikomboa Baitil Maqdis, na lau angeuliwa Umar رضي الله عنه basi moja kwa moja ukhalifa ungekuwa ni wa Ally رضي الله عنه, je kitendo hichi cha Umar رضي الله عنه kinaonyesha chuki na uadui kwa Ally رضي الله عنه? Na je kitendo cha Ally رضي الله عنه kuwa naibu wa Umar رضي الله عنه kinaashiria kuwa Umar رضي الله عنه ni dhalimu na ni muovu?

Hivi haijulishi kwa vitendo vyao hivyo kuwa kila mmoja anampenda mwenzake, anampa nasaha, na kwamba Ally رضي الله عنه alikuwa ni miongoni mwa watoa nasaha kwa Umar رضي الله عنه, na alikuwa miongoni mwa mawaziri wake walio thabiti, na kwamba Umar رضي الله عنه

mbele ya Ally رضي الله عنه ni Khalifa (kiongozi) mwema mwenye kuridhiwa?

11- Allah anasema:

﴿إِلَّا تَنصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ ٱللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ثَانِىَ ٱثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِى ٱلْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَٰحِبِهِۦ لَا تَحْزَنْ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا﴾

"Ikiwa nyinyi hamtamnusuru (Mtume ﷺ), basi Allah alishakwisha mnusuru walipomtoa walio kufuru, naye ni wa pili katika wawili walipokuwa katika pango, pale alipomwambia sahiba wake: Usihuzunike. Hakika Allah yu pamoja nasi"[1].

katika tukio ambalo huzingatiwa kuwa ni tukio kubwa katika uislamu ni Hijra (kuhama) kwake Mtume ﷺ kutoka Makka kwenda Madina, na aliye fuatana nae katika safari hiyo ni Abubakri رضي الله عنه, hivi (inawezekana vipi) Allah amchagulie Mtume wake (ﷺ) katika tukio hili kubwa mtu ambae hastahiki kufuatana nae? Hivi je Mtume ﷺ alishindwa kupata miongoni mwa Maswahaba zake mtu ambae ni mwema zaidi kuliko (kumchukua) mtu muovu dhalimu (kwa itikadi za Shia), au ni kuwa Allah alimchagua kwa ajili ya msafara huu mkubwa mtu (bora) anaestahiki kusuhubiana na Mtume wake (ﷺ)? Na kuwa kumchagua kwake Mtume ﷺ ni kwa kuzingatia kwamba

[1] Surat At Tawba/40.

huyo ni rafiki bora ambae mtu hupata hamasa kwake katika safari yake muhimu, na ikiwa Abubkri ﷺ ni mtu muovu dhalimu (kama wanavyoitakidi Mashia) basi vipi Allah amuweke pamoja Mtume wake mtukufu (ﷺ) na mtu huyu (muovu) kwa tamko la jam'u (kukusanya) katika kauli yake:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا﴾

[Hakika ya Allah yu pamoja nasi].

Ikiwa itikadi ya Mashia kwa Abubakri ﷺ ni sahihi, basi si ingekuwa bora aya isomeke:

(إِنَّ اللهَ مَعِيْ)

(Hakika ya Allah yu pamoja nami)?

12- Wanapokea Mashia kutoka kwa imamu Jafar Sswaadiq (muasisi wa madhehebu ya Jaafariy kwa mujibu wa itikadi yao), amesema kwa kujifaharisha:

(أَوْلَدَنِيْ أَبُو بَكْرٍ مَرَّتَيْنِ)

(Abubakri amenizaa mara mbili)

Kwa sababu nasaba yake inaishia kwa Abubakri ﷺ kwa njia mbili:

Njia ya kwanza: upande wa mama yake ambae ni Fatma bint Al Qaasim bin Muhammad bin Abibakri ﷺ.

Njia ya pili: upande wa bibi yake aliyemzaa mama

yake, Asmaa bint Abdur Rahmaan bin Abibakri (Asmaa) ambae ni mama wa Fatma bint Al Qasim bin Muhammad bin Abibakri رضي الله عنهم.

Kisha tunapata kuwa Mashia wanapokea kutoka kwa Jafar As Swaadiq riwaya za uwongo katika kumkanusha babu yake Abubakri رضي الله عنهم.

Swali: Vipi Jafar As Swaadiq ajifaharishe kwa babu yake Abubakri رضي الله عنهم halafu upande mwengine amtukane?! Mfano wa maneno kama haya yanatoka kwa mtu wa sokoni aliye mjinga, na haiwezekani kuwa yanatoka kwa imamu ambae Mashia wanamzingatia ni mtambuzi zaidi wa dini katika zama zake na ndio mcha Mungu wao. Na wala hakulazimishwa na yeyote si kwa kusifu wala kutia dosari, na baadhi ya vitabu vya Shia (Raafidhwah) vimetaja riwaya kutoka kwa Jafar As Swaadiq kwamba alimwambia mwanamke fulani ambaye alimuuliza kuhusiana na Abubakri na Umar رضي الله عنهما: **"Je nikiri ukhalifa wao?! akasema: ndio kubali (kuwa ni makhalifa), kisha akauliza tena: nitakapokutana na Mola nimwambie we**[1]we ndiye uliyeniamrisha nikubali kuwa wao Makhalifa?! Akamwambia: ndio".

Na pia vinaitaja riwaya kwamba **mtu mmoja**

[1] Angalia kitabu: (Raudhwatul Kaafi: J. 8, Uk. 101).

miongoni mwa wafuasi wa Baaqir alishangaa pindi alipomsikia Baaqir akimsifia Abubakri رضي الله عنه kuwa Swiddiiq, yule mtu akasema: Unamsifia kwa (kumuita) hivyo?! Baaqir akasema: ndio! Yeye ni Swiddiiq, na yule ambae hakubali kuwa yeye (Abubakri) ni Swiddiiq, basi Allah asiikubali kauli (maombi) yake huko akhera"[1], basi jee mashia wana rai gani kwa kwa Abuu Bakari Aswiddiiq رضي الله عنه?

13- Lau kafiri akizikwa kwenye makaburi ya waislamu, basi ni wajibu kwa waislamu kufukua kaburi lake na kumtoa katika makaburi ya waislamu. Na kwa mujibu wa itikadi ya Shia (Raafidhwah) Abubakri na Umar ni Makafiri Madhalimu, basi kwa nini Ally رضي الله عنه hakufukua makaburi yao na kulitoharisha kaburi la Mtume ﷺ na kua karibu nao, ikiwa kile wanachoitakidi Shia (Raafidhwah) ni sahihi? Au Mtume ﷺ ni dhalili kwa Mola wake mpaka kufanya kuwa waliozikwa pembeni ya kaburi lake ni Makafiri Madhalimu?

14- Dalili ya mafaniko ya Kiongozi au Mlezi yeyote yule na uwezo wake katika kuongoza ni kufaulu katika kuwalea wafuasi wake, kwa hiyo uwezo wa Mtume ﷺ katika malezi uko chini zaidi,

---

[1] Angalia kitabu: (Kashful Ghumma: J. 2, Uk. 360).

kiasi ya kuwa watu wengi aliyowalea wapo kinyume na malezi yake, na ilikuwa wafuasi wa kila Mtume ndio wabora katika watu wa Umma wao, lakini Mtume ﷺ amenyimwa sifa hiyo, pale ambapo wamekuwa watu waovu zaidi katika Umma wake ni Maswahaba zake isipokuwa idadi chache miongoni mwao? Hivi muislamu yeyote mwenye akili timamu ataridhia matusi haya juu ya Mtume ﷺ.

15- Kwa mujibu wa nukuu za vitabu vya Mashia vyenye kutegemewa, ni kwamba jamii ya Maswahaba ni jamii ya chuki na mizozo, baina ya kwamba Qu'an inatueleza kinyume na wanavyoitakidi Shia (Raafidhwah), Allah anasema:

﴿مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ ۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ ۖ﴾

"Muhammad ni Mtume wa Allah, na walio pamoja nae wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao"[1].

Na pia Allah anasema:

﴿وَٱذْكُرُوا۟ نِعْمَتَ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنتُمْ أَعْدَآءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِۦٓ إِخْوَٰنًا﴾

"Na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu, pale mli-

[1] Surat Muhammad/29.

pokuwa nyinyi kwa nyinyi ni maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu"[1].

Na Allah amesema:

﴿فَإِنَّ حَسْبَكَ ٱللَّهُ ۚ هُوَ ٱلَّذِىٓ أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِۦ وَبِٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾ وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ ۚ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا مَّآ أَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَٰكِنَّ ٱللَّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّهُۥ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾

"Basi Allah anakutosheleza. Kwani ndiye aliyekuunga mkono kwa nusura yake na kwa Waumini * Na akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungelitoa vyote viliomo duniani usingeliweza kuziunga nyoyo zao, lakini Allah ndiye aliyewaunganisha. Hakika yeye ndiye Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima"[2].

Kwa hiyo tumuamini nani, vitabu vya Mashia au Qur'ana? Kisha ikiwa hali ya jamii ya Maswahaba ni kama vinavyoeleza vitabu vya Mashia, basi iliwafikia vipi watu dini? Na vilevile ilienea kupitia mikono ya akina nani? Na ni akina nani walio simama kuikomboa miji na kueneza dini?

16- Kwa mujibu wa itikadi ya Shia (Raafidhwah), ni kwamba idadi kubwa ya Maswahaba wameritadi na

---

1 Surat Aal Imraan/103.

2 Surat Al Anfaal/62-63.

ni waovu, basi ni akina nani ambao zimeteremka aya za kuwasifia, mfano kauli ya Allah:

﴿وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلۡأَوَّلُونَ مِنَ ٱلۡمُهَٰجِرِينَ وَٱلۡأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحۡسَٰنٖ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُ وَأَعَدَّ لَهُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي تَحۡتَهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ﴾

"Na wale waliotangulia, wa kwanza, katika Muhajir-iina na Answaar, na walio wafuata kwa wema, Allah ameridhika nao, na wao wameridhika naye, na ame-waandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele, huko ndiko kufuzu kukubwa"[1].

Na pia anasema:

﴿لَّقَدۡ رَضِيَ ٱللَّهُ عَنِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ إِذۡ يُبَايِعُونَكَ تَحۡتَ ٱلشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمۡ فَأَنزَلَ ٱلسَّكِينَةَ عَلَيۡهِمۡ وَأَثَٰبَهُمۡ فَتۡحٗا قَرِيبٗا﴾

"Kwa hakika Allah amewaridhia waumini, pale wali-pokupa wewe Bai'a chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, basi akawalipa kwa (kuwapa) Ushindi wa karibu"[2].

Na kauli yake:

﴿مُّحَمَّدٞ رَّسُولُ ٱللَّهِۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلۡكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيۡنَهُمۡۖ تَرَىٰهُمۡ رُكَّعٗا سُجَّدٗا يَبۡتَغُونَ فَضۡلٗا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضۡوَٰنٗاۖ سِيمَاهُمۡ فِي وُجُوهِهِم مِّنۡ أَثَرِ ٱلسُّجُودِۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمۡ

---

1 Surat Tawba/100.

2 Surat Al Hashri/18.

فِي ٱلتَّوْرَىٰةِ[1] وَمَثَلُهُمْ فِي ٱلْإِنجِيلِ كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْـَٔهُۥ فَـَٔازَرَهُۥ فَٱسْتَغْلَظَ فَٱسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِۦ يُعْجِبُ ٱلزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلْكُفَّارَ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًۢا﴾

"Muhammad ni Mtume wa Allah, na walio pamoja nae wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Allah. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri, Allah amewaahidi walio amini na wakatenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa"[2].

Na kauli yake Allah aliposema:

﴿كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ﴾

---

1 Zingatia kauli ya Allah: ﴿مَثَلُهُمْ فِي ٱلتَّوْرَىٰةِ وَمَثَلُهُمْ فِي ٱلْإِنجِيلِ﴾, ni muhali Allah kuwasifu Maswahaba ndani ya vitabu vya Mayahudi na Manaswara, na kuwapigia wao mifano miwili mitukufu, hali ya kuwa anajua kuwa wataritadi, hakika hii ni dosari kwa Allah, kwa sababu Mayahudi watasema: "Allah ametuongope (Allah atuhifadhi), pale alipotaja sifa za watu wema, kisha watu hawa wameritadi?". Na aya hizi ni mfano wa upanga mkali juu ya yule mwenye judai ukafiri wa Maswahaba wa Muhammad ﷺ, Allah awaridhie.

2 Surat Muhammad/29.

"Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio teuliwa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Allah"[1].

Na aya nyingi zaidi ya hizi wachilia mbali hadithi za Mtume ﷺ, tumuamini nani, vitabu vya Mashia vinavyo watukana Maswahaba au Aya za Qur'an?

17- Allah anasema:

﴿لِلْفُقَرَآءِ ٱلْمُهَٰجِرِينَ ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِمْ وَأَمْوَٰلِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا وَيَنصُرُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ ﴿٨﴾ وَٱلَّذِينَ تَبَوَّءُو ٱلدَّارَ وَٱلْإِيمَٰنَ مِن قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِى صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِّمَّآ أُوتُوا۟ وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِۦ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾ وَٱلَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلْإِيمَٰنِ وَلَا تَجْعَلْ فِى قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾

"Wapewe mafakiri Muhajiriina waliotolewa majumbani mwao na mali zao kwa ajili ya kutafuta fadhila kutoka kwa Allah na radhi zake, na wanamnusuru Allah na Mtume wake. Hao ndio wakweli * Na wale walio na maskani na Imani kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa Muhajiriina, bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na

[1] Surat Al Imraan/110.

mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa[1].

Allah katika aya hizi amewagawa waislamu katika makundi matatu na hakuna kundi la nne, kundi la kwanza ni **"Muhaajiriina** (رضي الله عنهم)**"** na wameshakufa, kundi la pili ni **"Answaar** (رضي الله عنهم)**"** nao pia wameshakufa, kundi la tatu ni **"Wenye kuwaombea hao msamaha"**, kundi hili ni lenye kubakia mpaka siku ya kiama, je Shia atajiingiza kwenye kundi gani kati ya makundi haya matatu, hali ya kuwa yeye si **"Muhaajiriina"** wala si **"Answaar"** wala hayupo katika **"Wenye kuwaombea hao msamaha"**.

18- Mashia wanakubali Uslamu wa Maswahaba katika zama za Mtume ﷺ lakini wanadai kwamba waliritadi baada ya hapo**!** Ajabu iliyoje, vipi wamekubaliana juu ya kwamba Maswahaba wote waliritidi baada ya kufa Mtume ﷺ? Vipi wamnusuru Mtume ﷺ wakati wa shida na tabu, na kujitolea Nafsi pamoja na Mali zao, na wengine wameuliwa, kisha baada ya kufa Mtume ﷺ tu wakaritadi pasi na sababu yoyote ile**?!** Na ikiwa mtasema kuritadi kwao ni kwa sababu ya kumtawalisha kwao Abubakri رضي الله عنه, mtajibiwa: kwa

[1] Surat Al Hashri/8-10.

nini Maswahaba wote wa Mtume ﷺ wakubaliane kumtawalisha Abubakri رضي الله عنه, kwani walikuwa wanaogopa nini kwake? Je Abubakri رضي الله عنه alikuwa nguvu na mamlaka juu yao ya kuwalazimisha wampe Bai'a? kisha Abubakri رضي الله عنه ni Ukoo wa Bani Taym miongoni mwa Quraish, na walikuwa ni wachache kwa idadi miongoni mwa Makureish, na Makureish waliokuwa wengi kwa idadi ni Bani Haashim, Bani Abdi Ddaar, na Bani Mkhzuum.

Kwa hiyo hakuwa na uwezo wa kuwalazimisha Maswahaba wa Mtume ﷺ wampe Bai'a, basi ni kwa nini Maswahaba watoe muhanga jihadi yao, imani yao, kumnusuru kwao Mtume, kutangulia kwao katika Uislam, dunia yao na akhera yao kwa maslahi ya mtu mwengine ambae ni Abuubakri رضي الله عنه?

19- Kitu gani kilicho wapelekea Answaar kumpa Bai'a Abubakri رضي الله عنه, hali ya kuwa alishawaambia kwamba jambo hili (ukhalifa) uko mikononi mwa Makureish, na Answaar katika hili hawana nafasi?

20- Mara nyingi Maulamaa wa Shia (Raafidhwah) wanaelezea mapenzi ya Answaar (watu wa Madina) kwa Ally رضي الله عنه na kwamba wao walikuwa wengi katika jeshi la Ally رضي الله عنه katika vita ya Swiffiin. Tuwaambia: ikiwa ndio hivyo kwa nini wasimpe (Bai'a ya) ukhalifa

Ally رضي الله عنه na badala yake wakampa Abubakri رضي الله عنه**?!** hutapata jawabu lenye kukinaisha ambalo litaufurahisha moyo wako. Ndio maana tunaviona vitabu vya Mashia ambavyo vinawasifu Answaar na kusimama kwao bega kwa bega na Ally رضي الله عنه kwenye vita ya Swiffiin ndio hivyo hivyo vinavyotaja kwamba waliritadi na kurudi nyuma kwenye tukio la Thaqiifa**!**

21- Je Abubakri na Umar رضي الله عنهما wakati walipokaa katika utawala (walipokuwa makhalifa) ni kitu gani walikificha miongoni mwa sheria za dini? Na je Ally رضي الله عنه alipotawala alidhihirisha yale waliyoyaficha? Na ni mambo gani waliyoyazusha wakati wa ukhalifa wao kisha Ally رضي الله عنه alipotawala aliyaondosha?

22- Ikiwa Muawiya رضي الله عنه ni Kafiri na Mzandiki kama vilivyoandika vitabu vya Shia (Raafidhwah), kwa nini Husein رضي الله عنه alijiuzulu na kumuachia yeye madaraka**!** Bali akawa ni miongoni mwa raia waliochini ya mamlaka yake**!!** Hivi haizingatiwi kwamba kujiuzulu kwa Husein رضي الله عنه na kumuachia ukhalifa mtu Kafiri Mzandiki (kama wanavyodai Mashia) ni kutia dosari kulindwa kwake na kukosea (Ma'asuum)**!** Bali haizingatiwi kuwa ni uhalifu (kashfa) kwa raia wake ambao Allah alimpa ili awaongoze**!!** Hakika kitendo hiki cha Hasan رضي الله عنه kinajuilisha mambo mawili tu: Dosari kwake na kwamba yeye amefanya khiyana

kwa amana aliyopewa kwa kuacha uimamu wake, au ni kuwa Muawiya رضي الله عنه anastahiki kuwa Khalifa, na hivyo ndivyo alivyofahamu Hasan رضي الله عنه ndio maana akajiuzulu na kumuachia yeye ukhalifa.

23- Allah amesema:

﴿يَٰنِسَآءَ ٱلنَّبِيِّ لَسۡتُنَّ كَأَحَدٖ مِّنَ ٱلنِّسَآءِۚ إِنِ ٱتَّقَيۡتُنَّ فَلَا تَخۡضَعۡنَ بِٱلۡقَوۡلِ فَيَطۡمَعَ ٱلَّذِي فِي قَلۡبِهِۦ مَرَضٞ وَقُلۡنَ قَوۡلٗا مَّعۡرُوفٗا ٣٢ وَقَرۡنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجۡنَ تَبَرُّجَ ٱلۡجَٰهِلِيَّةِ ٱلۡأُولَىٰۖ وَأَقِمۡنَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتِينَ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَطِعۡنَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓۚ إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذۡهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجۡسَ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِ وَيُطَهِّرَكُمۡ تَطۡهِيرٗا ٣٣ وَٱذۡكُرۡنَ مَا يُتۡلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنۡ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ وَٱلۡحِكۡمَةِۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا﴾

"Enyi wake wa Nabii, nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine ikiwa mtamcha Allah, basi msilegeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake, na semeni maneno mema * Na kaeni majumbani kwenu, wala msitoke kutoka kijaahiliya (kama wakivyotoka wanawake kabla ya uislamu). Na shikeni Swala, na toeni Zaka, na mtiini Allah na Mtume wake. Hakika Allah anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni kabisa * Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika aya za Allah na hikima. Kwa hakika Allah ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye habari"[1].

[1] Surat Al Ahzaab/32-34.

Mfufulizo wa aya hizi ni mazungumzo wanayoelekezewa wakeze Mtume ﷺ, na kwamba aya zote hizi ikiwemo kauli ya Allah:

﴿إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذۡهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجۡسَ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِ وَيُطَهِّرَكُمۡ تَطۡهِيرٗا﴾

"Hakika Allah anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni kabisa"[1].

ni sehemu ya aya ambayo imeteremka kwa mama wa waumini, basi vipi mashia wanawatoa wakeze Mtume ﷺ katika aya hii kwa kutolea hoja hadithi ya Kisaa (kufunikwa nguo)? Je hadithi ya Kisaa (kufunikwa nguo) imekuja kuondosha makusudio ya aya hizo zilizopita au ni ziada na kubainisha ya kwamba aya ya kutakasa (Tatwhiir) inawaenea mpaka wasiokuwa wake za Mtume ﷺ, ili isije ikaeleweka kuwa inawahusu wao tu, kwa mujibu wa mpangilio wa maneno?

24- Katika aya hizi nane kuna maamrisho na makatazo:

Moja:

﴿فَلَا تَخۡضَعۡنَ بِٱلۡقَوۡلِ﴾

"Msilegeze sauti zenu"

---

[1] Surat Al Ahzaab/33.

Mbili:

﴿وَقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا﴾

"Na semeni maneno mema"

Tatu:

﴿وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ﴾

"Na kaeni majumbani kwenu"

Nne:

﴿وَلَا تَبَرَّجْنَ﴾

"wala msitoke (msijishauwe)"

Tano:

﴿وَأَقِمْنَ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

"Na shikeni Swala"

Sita:

﴿وَءَاتِينَ ٱلزَّكَوٰةَ﴾

"Na toeni Zaka"

Saba:

﴿وَأَطِعْنَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ﴾

"Na mtiini Allah na Mtume wake"

Nane:

﴿وَٱذْكُرْنَ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ﴾

"Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu" [1]

---

[1] Surat Al Ahzaab/32-34.

Na lau tukimuuliza muislamu yeyote mwenye akili: kwamba maamrisho yaliyokuja kwenye aya hizi kwa wake wa Mtume ﷺ nini makusdio yake? Bila shaka jawabu lake ni kwamba: **" ili watoharishwe wakeze Mtume ﷺ "** na Allah amebainisha sababu katika maarisho na makatazo hayo akasema:

﴿إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجْسَ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا﴾

"Hakika Allah anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni kabisa"[1].

Hakika maneno yalivyo ni kwamba: Enyi wake za Mtume ﷺ Allah amewapa maamrisho hayo na makatazo ili akuondoleeni uchafu na awatoharishe.

25- Hadithi ya Kisaa (kufunikwa nguo) inawahusu watu watano tu, kama ilivyotajwa katika hadithi, basi kwa nini Mashia wamewaingiza (wamewazidisha) watu wengine katika hadithi wasiokuwa hao watano, je alitaja Mtume ﷺ katika hadithi hiyo kwamba hao (waliozidishwa) nao pia ni Ahlul Bait wake, na watu tisa miongoni mwa watoto wa Husein رضي الله عنه na hakuna yeyote miongoni mwa watoto wa Hasan رضي الله عنه, kwa mpangilio uliomashuhuri kwa upande wa Shia Ithnaasharia? Kwa nini Mashia Ithnaasharia wame-

[1] Surat Al Ahzaab/33.

waingiza kwenye hadithi hii watu ambao Mtume ﷺ hakuwataja, wakati ambapo kuna watu wamewatoa (waohusika na hadithi hiyo) ambao Aya zimewaterемkia wao, nakusudia mama wa waumini (Allah awaridhie).

26- Hadithi ya Kisaa (kufunikwa shuka) imetajwa kwenye vitabu vingi vya kutegemewa kwa upande wa Ahlus Sunnah, isipokuwa kitabu kilicho sahihi zaidi (miongoni mwa hivyo) ni Sahihi Muslim, ambae amepokea hadithi hii kutoka kwa mama wa waumini Aisha رضي الله عنها, lau ingelikuwa msimamo wa Aisha رضي الله عنها kwa Ahlul Bait ni ki-adui kama wanavyodai Mashia, kwa nini asimulie hadithi hii ambayo inahesabika kuwa ni hoja dhidi yake, kwa mtazamo huo wa Shia? Na kuna maslahi gani kwa Aisha رضي الله عنها katika kuipokea hadithi hii?

27- Allah ameteremsha Aya za kumtakasa Aisha رضي الله عنهاkatika kisa cha Ifki (uwongo) ambacho ni mashuhuri na akasafishwa kutokana na ubaya huo, kisha tunapata baadhi ya Mashia wanaendelea kumsingizia yeye uovu[1]!! Tunajilinda kwa Allah, Na madai haya kama ilivyokuwa ndani yake kuna matusi dhidi ya Mtume ﷺ basi pia kuna matusi dhidi ya

[1] Tazama kitab: (Tafsirul Qummi: J. 2, Uk. 377) na (Tafsirul Burhaaniy: J 4, Uk. 377).

Allah Subhaanah ambae anajua ghaib (mambo yaliyofichika), na wala hakumfahamisha Mtume wake ﷺ kwamba mkewe ni mwenye khiyana (mzinifu)?! Ubaya ulioje wa madhehebu haya, wanawatusi wake wa Mbora wa viumbe ambao ni Mama wa waumini.

28- Vipi Mtume ﷺ azikwe katika chumba cha Aisha رضي الله عنها?! na hali ya kuwa Mashia wanamtuhumu kwa uzinifu na unafiki (Allah atulinde)?! Je haikuwa kuzikwa kwa Mtume ﷺ ndani ya chumba cha Aisha رضي الله عنها ni dalili juu ya mapenzi yake kwake?!.

29- Uimamu kwa Mashia unazingatiwa kua ni Nasswi (tamko la kisheria) kutoka kwa Allah, kama ilivyokuwa utume ni kwa tamko la kisheria (chaguo) kutoka kwa Allah, kwa hiyo haifai kwa imamu aliyeteuliwa na Allah (kwa Nasswi) na kulazimishwa kutii, kukitaa cheo hicho kinachotoka kwa Allah, pamoja na hivyo lakini tumempata Ally رضي الله عنه anakataa kuwa uimamu wakati alipopewa (cheo hicho) baada ya kuuwawa Uthman رضي الله عنه, pale aliposema wakati walipotaka kumpa Bai'a: **"Niacheni na mchagueni mwengine asiyekuwa mimi, hakika sisi ni wenye kulielekea jambo gumu[1]"**.

[1] Nahjul Balaagha: (Uk. 136).

30- Mashia wanadai kwamba tamko kuhusu Uimamu wa Ally رضي الله عنه na kustahiki kwake kuwa Khalifa limethibiti ndani ya Qur'an, lakini Maswahaba wamelificha (wamelifuta), haya ni madai ya uwongo; kwa sababu sisi tumepata kwamba Maswahaba hawakuficha hadithi ambazo hutumiwa na Mashia katika kutolea ushahidi juu ya ukhalifa wa Ally رضي الله عنه; mfano wa hadithi:

"Wewe kwangu mimi ni sawa na nafasi ya Haroun kwa Musa"

na nyengine miongoni mwa hadithi zenye kufana na hiyo, kwa nini hawakuzificha?!

31- Allah amesema hali ya kusifu Qur'an tukufu:

﴿وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ ٱلْكِتَٰبَ تِبْيَٰنًا لِّكُلِّ شَىْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ﴾

"Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinachobainisha kila kitu, na ni uongofu, na rehema, na bishara kwa waislamu[1].

Kisha akasema tena:

﴿مَّا فَرَّطْنَا فِى ٱلْكِتَٰبِ مِن شَىْءٍ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ﴾

"Na hatujapuuza Kitabuni (Lauhil mahfuudh) kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa"[2].

---

1 Surat An Nahli/89/

2 Surat Al An'aam/38.

Na pia amesema:

﴿لَّا يَأْتِيهِ ٱلْبَٰطِلُ مِنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِۦ ۖ تَنزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ﴾

"Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hikima, Mwenye kusifiwa"[1].

Ikiwa itikadi ya ukhalifa kwa maimamu (12) ni nguzo miongoni mwa nguzo za dini, anakufuru yule ambae haitakidi hivyo, kwa nini Allah hakuutaja katika katika kitabu hichi (Qur'an), ijapokuwa kwa aya moja tu iliyo wazi, ikaondoa utata, na ikawa (aya hiyo) ni hoja ambayo itarejewa wakati wa kutafautiana, na wakati huo (ndani ya Qur'an) hutajwa mambo ambayo daraja yake ni ndogo kuliko daraja ya uimamu, kama mirathi, hukumu za ndoa, mikataba, mambo ya hedhi na nifasi na kuwinda na mambo mengine?.

32- Mashia wanadai kwamba Ally رضي الله عنه alimpa bai'a Abubakri kwa kulazimishwa, tujalie ni sawa ilikuwa hivyo, lakini Ally رضي الله عنه vilevile alimpa bai'a Umar kwa hiyari yake pasi na kulazimishwa, na dalili juu ya hilo ni kwamba Ally رضي الله عنه alikuwa waziri wa Umar رضي الله عنه, na alikuwa miongoni mwa washauri wake, mpaka Umar رضي الله عنه akasema: **"Najilinda kwa Allah kutokana na**

[1] Surat Fusswilat/42.

masuala mazito ambayo hakuwepo Abul Hasan (Ally رضي الله عنه)", hili linalazimu kuwa Abubakri na Umar رضي الله عنهما walikuwa ni maimamu waongofu, lau wangelikuwa ni viongozi madhalimu kama wanavyodai Mashia basi Ally رضي الله عنه asingekubali hali hiyo, kwa sababu mwenye kumsaidia dhalimu anakuwa mfano wake (katika adhabu), Allah anasema:

﴿وَلَا تَرْكَنُوٓاْ إِلَى ٱلَّذِينَ ظَلَمُواْ فَتَمَسَّكُمُ ٱلنَّارُ وَمَا لَكُم مِّن دُونِ ٱللَّهِ مِنْ أَوْلِيَآءَ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ﴾

"Wala msiwategemee wanaodhulumu, usije ukaguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Allah, wala tena hamtasaidiwa" [1]

33- Imekuja katika kitabu: (Nahjul Balaagha) ambacho Mashia wanakitukuza:

Miongoni mwa barua alizoandika Ally رضي الله عنه kwenda kwa Muawiya رضي الله عنهما: **"Hakika wamenipa Bai'a (kiapo cha utiifu) mimi watu ambao walimpa Bai'a Abubakri, Umar na Uthman, kwa yale ambayo waliwapa Bai'a wao juu yake,** kwa hiyo haikuwa kwa aliyehudhuria khiyari wala kwa asiyekuwepo kupinga, kwa sababu shura (inayozingatiwa) ni ya Muhaajiriina na Answaar, wakikubaliana kumchagua mtu na wakamuita kuwa

[1] Surat Hud/113.

ni imamu basi linakuwa jambo hilo Allah ameliridhia, na ikiwa mtu yeyote atatoka kwenye makubaliano yao, kwa kutia dosari au kuzusha bidaa watamrudisha kwenye lile alililoliacha (makubaliano), na akikataa watampiga vita kwa sababu ya kuifuata isiyokuwa njia ya waumini, na Allah atamuongoza huko ambako ataelekea, nakuapia kwa Allah ewe Muawiya endapo utatafakari kwa akili yako pasi na kufuata matamanio ya nafsi yako utanikuta mimi niko mbali na damu ya Uthman رضي الله عنه, na utafahamu kuwa mimi nilikuwa nimejitenga nae, isipokuwa kama utafanya jinai na hilo litakua ni jinai lako, wasalaam."[1].

Katika hili kuna dalili ya kwamba:

1- Imamu anachaguliwa na Muhaajiriina na Answaar; kwa hiyo hana yeye mahusiano yoyote na nguzo ya Uimamu kwa Mashia!.

2- Ally amepewa Bai'a (amechaguliwa) kwa njia ile ile ambayo alichaguliwa Abubakri, Umar na Uthman رضي الله عنهم.

3- Shura (inayozingatiwa) ni ya Muhaajiriina na Answaar, hili linajulisha juu ya fadhila na cheo chao kikubwa mbele ya Allah, na hali hiyo inapingana na na kutafautiana na taswira wanayoitoa Mashia kuhusu watu hao.

---

[1] Angalia kitabu: (Swafhat shuruuhi Nahjil Balaagha: Uk. 593).

4- Makubaliano ya Muhaajiriina na Answaar, ridhaa yao, na Bai'a yao kwa mtawala wao ndio ridhaa ya Allah, kwa hiyo hapo hakuna masuala ya kupora Uimamu kama wanavyodai Mashia, na kama ni kweli basi vipi Allah aliridhie na jambo hilo?!.

5- Halafu Mashia wanamlani Muawiya رضي الله عنه lakini hatujapa kwa Ally رضي الله عنه katika barua yake kuwa anamlani Muawiya رضي الله عنه.

34- Ikiwa Hasan رضي الله عنه ni imamu aliteuliwa na Allah, vipi ajiuzulu (atoke madarakani) na kumwachia mtu mwengine nafasi hiyo!

35- Ikiwa Hasan رضي الله عنه ni Ma'asuum (amekingwa na kutenda dhambi) basi itakuwa kujiuzulu kwake na kumwachia nafasi hiyo Muawiya رضي الله عنه ni jambo la haki na ni sawa hakuna ndani yake makosa yoyote, kama alivyokuwa yeye ameridhiwa na Allah basi Ma'asuum hawezi kufanya jambo lolote ambalo Allah haliridhii, lakini vitabu vya kutegemewa vya Mashia vinataja ya kwamba Husein رضي الله عنه ambae ni Ma'asuum wa pili baada ya Hasan رضي الله عنه alichukia jambo hili kwa ndugu yake, amesema Abu Mikhnaf: **"Alikuwa Maulana wetu Husein ibn Ally عليه السلام anadhihirishwa kuchukia kitendo cha kaka yake Hasan عليه السلام pamoja na Muawiya, na akisema: (kukatwa pua yangu kwa kiwembe inapendeza**

zaidi kwangu mimi kuliko kitendo alichofanya kaka yangu[1] kwa hiyo itakuwa kitendo alichofanya Hasan ﷺ ni makosa na wala si ridhaa itokayo kwa Allah, ndio maana Husein ﷺ akachukia, na hili linajulisha kuwa Hasan si Ma'asuum, kwa sababu Ma'asuum hafanyi kosa, hasa katika jambo linalohusu uongozi

(Uimamu), au atakuwa Husein ﷺ si Ma'asuum, kwa sababu amechukia jambo lililofanywa na Ma'asuum ambae hakosei, na hakuna analofanya isipokuwa ni sahihi.

36- Je Huesein As Shahiid alitoka kwa matashi yake tu au kwa sababu ya barua zilizomfikia kutoka kwa viongozi wa wafuasi wake! Kisha kwa nini

---

[1] Ameitaja Abul Hasan Al Irbiiliy katika kitabu chake: (Kashful Ghumma fii Ma'arifatil Aimma: J. 2, Uk. 205) kisha akazitaja beti zinazo ashiria juu ya jambo hilo:

Hakuna kitu kimenichukiza kama alivyonichukiza ndugu yangu
Na wala sijaridhia kwa ajili ya Allah kwa lile alilofanya

Lakini ikiwa Allah ameshapitisha hukumu yake
Hakuna budi lazima siku moja utaliona jambo hilo ni lenye kutokea

Lau mimi ningeshauriwa katika jambo hili basi wangeli muona
jamaa yao yuko mbali kabisa na jambo hili

Na nisingeridhia kwa lile ambalo wamelidhia wao
Hata kama wangelinipinga watu wote

Na lau ingelikatwa pua yangu kabla ya hapo
Kwa kiwembe nisingelikubali kufuata suluhu

wamnyime nusra baada ya kuwa wamemuita! Na jambo la ajabu hawa viongozi (waliomuita) ndio waliokuwa makamanda wa jeshi ambalo lilimuuwa yeye na Ahlul Bait wake.

37- Jambo gani lililo bora kwa maslahi ya umma, kujiuzulu kwa Husein رضي الله عنه na kumuachia uongozi (ukhalifa) Muawiya رضي الله عنه na kupatikana kwa Amani, au kutoka kwa Husein رضي الله عنه na yale yaliyotokea kwa sababu yake miongoni mwa misiba mingi, na lililo kubwa zaidi ni kumwagwa damu yake na damu ya Ahlul Bait watukufu, kisha yaliyojiri baada ya hapo kama tukio la Harra na kuzingirwa (kuwekwa kizuizini) Al Ka'ba, kisha lipi ni sahihi kuandikiana Mikataba na Muafaka kama alivyofanya Hasan رضي الله عنه pamoja na kuwa alikuwa anaweza kupigana na ana watu wengi, au kutoka na kupigana pamoja na kutokuwa na uwezo na uchache wa watu, kama alivyofanya Husein رضي الله عنه? Hakuna shaka mmoja wao atakuwa amepatia na mwengine amekosea, haiwezekani mambo hayo mawili kuwa ni sawa, na mwenye kukosea atakuwa si Ma'asuum kwa mujibu wanavyoelezea Shia maana ya Ma'suum.

38- Vitabu vya Mashia vinaeleza kwamba Mtume ﷺ alikuwa anawahusisha Ahlul Bait kwa

kuwafundisha elimu (maalumu) kinyume na Maswahaba wengine, kama vile (Msahafu wa Fatma, Jufri na mengine), hivi kweli jambo hili anastahiki kusifika nalo Mtume ﷺ aliyetumwa kwa watu wote! Allah anasema:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا رَحۡمَةٗ لِّلۡعَٰلَمِينَ﴾

"Nasi hatukukutuma ila ni Rehema kwa Walimwengu wote"[1]

Na amsema:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا كَآفَّةٗ لِّلنَّاسِ بَشِيرٗا وَنَذِيرٗا وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعۡلَمُونَ﴾

" Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri na mwonyaji, lakini watu wengi hawajui " [2]

39- Mashia wanaizingatia hadithi ya **Ghadir Khum** ni miongoni mwa dalili kubwa zinazojulisha kuwa ukhalifa (uimamu) umetajwa kuwa ni kwa Ally ibn Abi Twalib رضي الله عنه, je Ally رضي الله عنه aliwahi kumtolea hoja Abubakri رضي الله عنه na Maswahaba wengine kwa kuitumia hadithi hii kuwa ni dalili juu ya ukhalifa wake? Na lau tukubali kwamba Ally رضي الله عنه ameamrishwa kunyamaza kwa yale yatayompata, kwa nini basi alinyamaza pia Salmaan, Abu Dharri Miqdad na Ammaar na

---

1 Surat Al Anbiyaa/107.

2 Surat Saba'/28.

wengine miongoni mwa Maswahaba ﷺ ambao Mashia wanawazingatia kuwa wanaukubali ukhalifa wa Ally ﷺ kinyume na wengine? Je na hao pia wameamrishwa kunyamaza kwa yale yanayomsibu Ally ﷺ?

40 - Msimamo wa mashia kwa Hassan bin Ally ﷺ ni msimamo hasi kabisa kwa sababu ya kumuachia ukhalifa Muaawiya ﷺ, lakini hawawezi kumtusi kwa sababu ni miongoni mwa watu wa kisaai, endapo watamsema vibaya hoja yao ya kwamba watu wa kisaai wamekingwa na makosa itaporomoka. Lakini msimamo wao mbaya umejitokeza wazi pale walipo kizuwia kizazi chake kushika uimamu na badala yake maimamu wakawa wanatokana na kizazi cha Hussein ﷺ peke yake, bali baadhi ya mashia wamefikia wamefikia kusema kwamba: Watoto wa Hassan ﷺ walikuwa na matendo machafu ambayo hayawezi kabisa kuchukuliwa kwamba yamefanywa kwa Taqiyya.

41- Vimetaja vitabu tegemewa vya mashia kwamba Maimamu hawafikiwi na kero isipokuwa kwa khiyari yao, na wala hawafi mpaka watake wenyewe, na hayo yameelezwa na Alkulainiy katika kitabu chake Alkaafiy (Hakika ya maimamu wanatambua

lini wanakufa, na wao hawafi isipokuwa kwa hiyari zao), Basi kama ni hiyvo kuna haja gani ya Taqia kwao wao?

42- Hakika itikadi yao ya taqia na Isma (utoharifu na kukingwa na madhambi) havikusanyiki sehemu moja viwili hivyo, kwani taqia ima ni kunyamaza usiseme haki au ni kuinyamazia batili, na huku ni kuitia ila Isma, kama ambavyo taqia inatofautiana na dalili za Qur'an na Sunnah na hata athari zenye kupokelewa kutoka kwa Ahlil Bait (radhi za Allah ziwaendee), ambazo zinahimiza juu ya uvumilivu wakati wa shida na kuthibiti katika misingi ya haki, hata kama atafikwa na maudhi makubwa. Na katika dalili za hayo ni hadithi ya Ally رضي الله عنه: (Vipi nyinyi mtakapofikiwa na zama ambazo hukmu za Allah hazitotekelezwa, na mali kupewa baadhi ya watu tu na kunyimwa wengine, watakapofanyiwa uadui vipenzi wa Allah, na kupendwa maadui wake? Pakasemwa: Ewe Amiri (Kiongozi)wa waislamu ikiwa zama hizo zitatukuta jee sisi tufanyeje? Kasema:

(Kuweni kama (Maswahaba) wa Issa عليه السلام wamepasuliwa kwa misumeno, na wakasulubiwa juu ya mbao. Kufa katika utiifu wa Allah عز وجل ni bora kuliko kuishi katika kumuasi).

43- Na kama taqia ina nafasi ambayo imeelezwa na vitabu vya mashia vyenye kutegemewa, kwa nini hakuitumia Mjumbe wa Allah ﷺ katika mazingira magumu, bali imethibiti kwake ﷺ kwamba ilipoteremka kauli ya Allah:

﴿وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ ٱلْأَقْرَبِينَ﴾

:[*Na uwaonye jamaa zako wa karibu nawe*]

Ashuaraai: 214.

Alipanda Mtume ﷺ juu ya jabali Aswafaa na akawaita Makuraishi mchana pahala pa wazi si pakujificha, kama ambavyo katika vita vya Hunaini alielekea kwa maadui peke yake na huku anatangaza kwa sauti ya juu kabisa:

"Mimi ni Nabii sina uongo....Mimi ni mwana wa Abdulmutwalib".

Ingelikua Mtume ﷺ amekuja na taqia katika sharia yake jee si angestahiki zaidi kuiitumia katika nyakati hizo ngumu alizokumbana nazo bila ya kuingiza nafsi yake na masahaba wake ndani ya matatizo. Na kwa nini hakuitumia Huseini رضي الله عنه, na kukubaliana na hukmu ya Ibnu Ziyaadi kwa kufanya (Taqiya) tu ili apate kuihami damu yake na damu ya watu wake na wafuasi wake wa karibu?

44- Wanapokea mashia katika vitabu vyao, riwaya

zenye kupingana kutoka kwa maimamu wao katika maswala ya furui (mambo ya kifiqhi), mara anasema imamu Fulani: Jambo hili hukumu yake ni haramu, mara ni makuruhu, mara ni mubaha, mashia wanapoambiwa kua haya yanapingana, husema kuwa Imamu amesema hivyo kwa kutumia taqia, na kila muislamu anajua kuwa tofauti katika mas-ala ya kifiqhi ni jambo linakubalika, kunahaja gani kwa Imamu maasuum ya kujizonga kwa kile kinachoitwa taqiya?

45- Vinaeleza vitabu tegemewa vya mashia kwamba maimamu hawafi mpaka watake wenyewe, kama ilivyotajwa kwenye riwaya hii:

(Hakika ya maimamu wanatambua lini watakufa, na wao hawafi isipokuwa watake wenyewe) wakati huo huo vitabu hivyo vinaeleza kwamba hakuna imamu aliekufa kifo cha kawaida bali wote hufa kwa kuuwawa au kupewa sumu. (Hakuna imamu aliekufa kifo cha kawaida bali huuwawa au hupewa sumu). Sasa kwanini imamu ajichagulie kifo cha namna hii, jee huku si kujiuwa ambako kumeharamishwa?

46- Hakika ya Ally رضي الله عنه ameuwawa wakati ambao uma unamuhitajia sana, kutokana na fitina ambazo zilikua zinaendelea, sasa inakuaje kwa Ally ajichagulie

kuuwawa wakati kama huu ambapo raia wake wanamu hitajia? Na matokeo ya kufa kwake ni mwanawe Hassan رضي الله عنه kuachia ngazi na kumpisha Muaawiah رضي الله عنه awe ndie Kalifa mtu ambae Mashia wanamfanya kua ndie kiongozi mkuu wa ukafiri na utwaaghuti?

47- Vitabu vya mashia vinaeleza mambo ya maajabu mbali mbali ambayo yalikua yanajitokeza kwa ahlul baiti kwa mfano tu yale aliyoyaeleza Alhasan Aswafaar aliekufa 290 H. katika kitabu chake (Baswaair-darajaat) mfano: (**Mlango unaohusu maimamu, kuwa na uwezo wa kumpeleka mtu sehemu wanyotaka ardhini kwa uwezo waliopewa na Allah**) na (**Mlango kuhusu kupanda mawinguni Amiiril muuminiin رضي الله عنه na kupanda kwake katika sayari**) na (**Mlango unaohusu kumsifu Mjumbe wa Allah [ﷺ] na maimamu kwa uoni waliopewa wakuona mambo wakiwa macho au wamelala kinyume na watu wengine**) na mengineyo. Na kama haya ni ya kweli kwanini hawakujiondoshea kero walizokabiliana nazo, Ally رضي الله عنه aliuliwa kwa hadaa, na Hassan رضي الله عنه waliuliwa watu wake mbele ya macho yake, na kama ana maajabu kwanini asimkinge mtoto wake mchanga na mkuki uliompiga na kumuuwa mapajani pake? Ni kweli kwamba Ahlul Bait wanayo makarama hilo halipingiki lakini wasinasibishwe na miujiza na mazinga.

48- Utambulisho wa imamu kwa mashia ni:- (Mwanadamu ambae ana utawala wa ujumla wa mambo yote ya dini na dunia kwa niaba ya Mtume ﷺ, jee maana hii ya imamu inawafikiana na Mahadi asiekuwepo?

49- Imekuja katika hadithi ya Mahadi: (Lau kama itabakia siku moja tu duniani basi Allah angeifanya siku hiyo kuwa ndefu na kumleta mtu katika jamaa zangu ambae jina lake linafanana na langu na jina la baba yake linafanana na la baba yangu, Na kama tunavyojua kua Mjume wa Allah jina lake ni Muhammadi bin Abdillah ﷺ lakini Mahdi wa mashia jina lake ni Muhammad Ibni Al Hasan! Huu ni mushkeli mkubwa!

50- Mashia wanasema kwamba sababu ya kujificha imamu wao wa kumi na mbili ni kuwaogopa madhalimu, basi kwa nini kujificha huku kuendee wakati hatari haipo tena na dola mbali mbali za kishia kwa mujibu wa historia zilishawahi kutawala kwa mfano, dola ya Abiidiyyiina na Buwayhiyyiina na Swafawiyyiina na ya mwisho ni dola hii ya Irani iliyopo hivi sasa?!

Basi kwa nini hatokei hivi sasa ambapo mashia wana uwezo wa kumnusuru na kumlinda nchini

mwao?! Na wakati idadi yao hivi sasa ni mamilioni ya watu, na wao wanajitoa fidia kwake kwa roho zao asubuhi na jioni...!!

51- Wanadai mashia kwamba Mahdi wao atakapo dhihiri atahukumu kwa hukumu ya Al-daauud! Jee ipo wapi sheria ya Muhammad ﷺ inayofuta sheria zilizotangulia?!

52- Kwanini atakapokuja Mahdi wa mashia atatengamana na mayahudi na wakristo na kuwauwa waarabu na makuraishi?!! Hivi kwani Muhammad ﷺ si katika makuraishi na katika waarabu, na vilevile maimamu kwa mujibu maneno yao nao si ni katika waarabu?!

53- Wanapokea mashia kutoka kwa Abii Abdillah-Jaafari Asswaadiq- amesema: (Mwenye utawala baada yangu ni mtu ambae hamuiti kwa jina lake isipokua kafiri...) Na wanapokea kutoka kwa Abii Muhammad Alhasan Al-askariy kwamba amesema kumwambia mama yake Almahdiyyi: «Utabeba ujauzito wa mtoto mwanaume jina lake ni Muhammad nayeye ndie kiongozi baada yangu mimi....» Jee huku si kupingana ?! Mara munasema: Atakae mwita kwa jina lake ni kafiri, mara munasema kwamba Alhasani Al-askariy amemwita Muhammad!!

54- Wanadai wanazuoni wa mashia katika vitabu vyao vya asili kwamba Faatimah ﵂ alidhalilishwa, akapigwa, kavunjwa mbavu zake na mimba yake ya mtoto wake Muhsini ikaharibika. Jee yupo wapi shujaa Ally﵁ na matukio hayo?! Wapo wapi Banii Haashim wakubwa wa waarabu na wasio kuwa waarabu, mashujaa wa zama za kabla ya uislamu na baada ya uislam wakati hayo yanatokea?! Wapo wapi wafuasi wa Ally akina Abii Dhari, Salmani na Miqdaadi wakati wa matukio hayo! Wapo wapi maswahaba na jamaa wengine wa Mtume s.w.a?!

55- Mashia wanadai kwamba Mtume ﷺ alimwambia Ally﵁ mambo yatakayo mpata Fatma ﵂, na akamtaka anyamaze juu ya hayo yote, na sehemu nyingine vitabu vya Mashia na vya Ahlus Sunnah vinaelezea kwamba Mtume ﷺ alikasirika akasimama kuwahutubia watu, pale aliposikia kwamba Ally﵁ anataka kumuoa mtoto wa Abu Jahli, Mtume ﷺ**"Fatmah ni sehemu ya mwili wangu, na mimi nachukia kumfanyia yeye ubaya**[1], kwa ajili ya kuchunga asije kukasirika Fatma ﵂ asikachukie, basi vipi Mtume ﷺ amuamrishe Ally﵁ anyamaze juu ya kupigwa kwa Fatma ﵂ na kumuua, wakati

[1] Bukhari na Muslim.

amemzuia kuoa jambo ambalo ni halali kwake, kwa kuchunga tu Fatma ﵂ asije akaudhika? Kisha madai ya Mashia kwamba Mtume ﷺ amemuamrisha Ally ﵁ asimuhami mkewe na heshima yake, ni jambo ambalo haliwezekani kiakili wala kisheria, kwa sababu Mtume ﷺ ameamrisha mtu kutetea mali na familia yake, akasema: **"Mwenye kuuawa kwa kuhami mali yake basi huyo ni shahidi, na mwenye kuuawa kwa kuihami familia, damu au dini yake huyo ni shahidi [1]"**.

Na katika mapokezi mengine imekuja ndani ya vitabu vya Mashia kwa matamshi mbali mbali, miongoni mwake: **"Mwenye kuuawa kwa dhulma kwa kuwahami watu wake basi huyo ni shahidi, na mwenye kuuawa kwa dhulma kwa kuihami mali yake huyo ni shahidi, na mwenye kuuliwa kwa kumtetea jirani yake huyo ni shahidi, na mwenye kuuawa katika dhati ya Allah basi huyo ni shahidi",** Je ni kweli Mtume ﷺ awaamrishe waislamu wote kulinda mali zao na wake zao, kisha amkataze Ally ﵁ kumuhami ahli wake ambae ni mwanamke bora alieruzukiwa na Allah Faatimah mbora wa wanawake wa ulimwengu? Bali uma wa Muhammad ﷺ umeamrishwa kuwatetea wanawake wote wa ki-islamu, seuze wanawake wa nyumba ya Mtume ﷺ.

---

[1] Sunan Abi Daud.

56- Suala la kuhusiana na (bustani ya) Fadak:

Vimetofautiana vitabu vya Mashia kuhusu madai ya Fatma رضي الله عنها kupewa (bustani ya) Fadak, baadhi ya vitabu vimeeleza kwamba yeye Fatma رضي الله عنها anadai haki yake kwenye kumrithi baba yake, lakini la ajabu ni kwamba katika fiqhi ya Mashia mwanamke harithi ardhi, Al Kulaini ameweka mlango maaalu kwenye kitabu cha (Al kaafi) wenye anuani: **"Hakika wanawake hawarithi chochote katika mali ya mashamba"**, na ametaja ndani ya mlango huo kutoka kwa Abi Jafar amesema: **"Wanawake hawarithi chochote katika ardhi na shamba**[1]. Na amepokea Attwuusiy katika kitabu chake Attahdhiib[2] kutoka kwa Maysir amesema: "Nimemuuliza Abu Abdillah عليه السلام kuhusiana na wanawake wanapata nini katika mirathi? Akasema wao wanapata thamani ya matofali, majengo, mbao na miti basi, ama ardhi (viwanja) na mashamba hakuna ndani yake fungu lao la mirathi".

Na baadhi ya vitabu vimetaja kuwa bustani ya Fadak Mtume ﷺ aliitoa sadaka kumpa Fatma رضي الله عنها, Imepokewa kutoka kwa Abi Abdillah amesema: Baada ya kufa Mtume ﷺ na Abubakri رضي الله عنه akashika ukhalifa,

---

[1] Angalia kitabu: Furuul Kaafi: (J. 7, Uk. 127) cha Al Kulaini.

[2] Angalia kitabu: Tahdhiibul Ahkaam: (J. 9, Uk. 254).

alituma ujumbe kwenda kwa wakili kwa Fatma ﵂ ili akamtoe (katika shamba) huko Fadak, Fatma ﵂ alimwendea na akamwambia: Ewe Abubakri, umedai kwamba wewe ni khalifa wa baba yangu, na umemtuma mjumbe kwenda kumtoa wakili wangu huko Fadak, hali ya kuwa unafahamu kwamba Mtume ﷺ alilitoa sadaka kwangu mimi, na mimi kwa hilo ninao mashahidi, Abubakri﵁ akasema: Mtume ﷺ harithiwi. Fatma ﵂ akarudi kwa Ally﵁ na kumueleza, Ally﵁ akamwambia rudi ukamwambie: **"Umedai kwamba Mtume harithiwi, wakati Sulaiman alimrithi Daud, na Yahya alimrithi Zakaria, kwanini mimi nisipate mirathi ya baba yangu?"**[1].

Katika kisa hichi kuna mgongano wa wazi, mwanzo wa kisa kinaeleza kwamba Fadak ni wasia wa Mtume ﷺ kwa Fatma ﵂, lakini Abubakri﵁ alimjibu kwamba Mtume ﷺ harithiwi, na suali lake la kurudi tena kwa Abubakri﵁ na kumwambia **"vipi nisimrithi baba yangu?"**, mjadala unazunguka katika jambo la mirathi, na hakushindwa Fatma ﵂ kumwambia Abubakri﵁ kwamba **"mimi nakueleza kuhusu wasia na wewe unazungumzia mirathi, hilo halihusiani na hili?".**

57- Ikiwa Fadak ni zawadi ambayo Mtume ﷺ

[1] Angalia kitabu Al Ikhtiswaas: (Uk..) cha Al Mufiid.

alimpa Fatma ﵂, je Mtume ﷺ alimpa bint yake Ummu Kulthuumu ﵂ mfano wa kile alichompa Fatima? au alimshirikisha katika kile ambacho alimpa yeye Fatima? Kwa sababu Ummu Kulthuumu alikuwa yupo hai, wakati Allah alipompa ushindi Mtume wake ﷺ na kuikomboa Fadak na Khaibar, na Ummu Kulthuum alifariki mwezi shaaban mwaka wa 9[h.]

Jee inawezekana vipi Mtume ﷺ asifanye uadilifu baina ya watoto wake, hali ya kuwa yeye mwenyewe amesema:

"Ikiwa mimi sikufanya uadilifu, basi ni nani atakae fanya uadilifu?".

Kutoka Nuumaan bin Bashiri﵁ kasema kwamba baba yake alikwenda nae kwa Mtume ﷺ na kumwambia kwamba ''nimempa zawadi mtoto wangu huyu yule mtumwa wangu, Mtume ﷺ akamuuliza, je watoto wako wote umewapa kama ulivyompa huyu? akasema hapana, Mtume ﷺ akamwambia mrejeshe [1].

Je inawezekana vipi Mtume ﷺ akataze jambo kisha yeye alifanye jambo hilo hilo? Je inawezekana Mtume ﷺ afanye jambo ambalo amelihesabu kuwa ni kufanya dhulma baina ya watoto?

---

[1] Bukhari, angalia Fat'hul Baari: (J. 5, Uk. 211).

58- Wakati Ally رضي الله عنه alipokamata ukhalifa aliifanya nini hii bustani ya Fadak? Je aliigawa kwa warithi wa Fatma رضي الله عنها au aliibakisha katika hali ile ile aliyo iweka Abubakri رضي الله عنه?.

59- Mashia wanadai kwamba hakuna aliekusanya Qur'an kama ilivyo teremshwa isipokuwa Ally رضي الله عنه, lakini aliificha kwa kuchelea fitna, na ili watu wasije wakaritadi, Lakini alishiriki kwenye kuwapiga watu vita chini ya bendera ya Abubakri kwa jambo dogo kuliko hilo! na wala hakuchunga na kuogopa kwamba watu wasije wakaritadi, kwa sababu Ally رضي الله عنه alikuwa mbele katika jeshi ambalo liliwapiga wale wenye kuzuia zaka, kisha je Ally رضي الله عنه pindi aliposhika ukhalifa aliidhihirisha hiyo Qur'an ambayo anaihifadhi yeye tu peke yake?

60- Je Ahlul Bait wana kitabu kingine kisicho kuwa Qur'an ambacho huchukua elimu yao kwenye kitabu hicho? na kuna faida gani ya vitabu vyengine vinavyotajwa ndani ya vitabu vya kutegemewa vya Mashia? Mfano: (Msahafu wa Fatima, Al Jaamiu, Swahiifatu Nnaamuus, Swahiifatu Dhuaabati Sseif, Swahiifatu Ally, Al Jufri, Taurat, Injili, na Zaburi?)

61- Mashia wanapinga tamko la kupotoshwa kwa Qur'an hii iliyo mikononi mwetu, na wanasema huo ni

miongoni mwa uzushi wa Ahlus Sunnah dhidi yao, basi wanasemaje kuhusu matamko haya yaliyo ndani ya vitabu vyao vyenye kutegemewa: Kutoka kwa Abu Abdillah amesema:

(ومن يطع الله ورسوله في وِلَايَةِ عَلِيٍّ وولاية أَئِمَّةٍ من بعده فقد فاز فوزا عظيما)

Na mwenye kumtii Allah na Mtume wake kuhusu Utawala wa Ally na Utawala wa Maimamu baada yake hakika amefaulu kufaulu kukubwa) kisha akasema: hivi ndivyo ilivyoshuka [1]

Na kutoka kwa Abu Jafar amesema ameteremka Jibril (alayhis salaam) na aya hii kwa Muhammad kama hivi:

(بِئْسَمَا اشْتَرَوا به أنفسَهم أنْ يكفُرَوا بما أنزل الله في عَلِيٍّ بَغْياً)

Ubaya ulioje waliozi nunulia nafsi zao, kuwa kukufuru yale aliyo teremsha Allah kuhusu Ally, hali ya kumfanyia uadui[2].

Na kutoka kwa Jabir amesema: Ameteremka Jibril ﷺ na aya hii kwa Muhammad kama hivi:

(وإِنْ كنتم في ريب مما نزلنا على عبدنا في عَلِيٍّ فأتوا بسورة من مثله)

---

[1] Angalia kitabu: Usuulul Kaafi: (J. 1, Uk. 414).

[2] Angalia kitabu: Usuulul Kaafi: (J. 1, Uk. 417).

Na mkiwa nyinyi ni wenye shaka katika lile tuliloteremsha juu ya mja wetu kuhusu Ally basi leteni sura iliyo mfano wake [1]

Na kutoka kwa Abu Abdillah (عليه السلام) amesema: Jibril aliteremka kwa Muhammad ﷺ na aya kama hivi:

(يا أيها الذين أوتوا الكتاب آمنوا بما نزَّلنا في عَلِيٍّ نورا مبينا)

Enyi mliopewa kitabu, aminini yale tuliyoteremsha kuhusu Ally, kuwa ni nuru yenye kubainisha [2]

Muhammad bin Sinan kutoka kwa Arridhwaa (عليه السلام) amesema:

(كَبُرَ على المشركين بولاية عَلِيٍّ ما تَدْعُوهم إليه يا محمد من ولاية عَلِيٍّ)

Ukubwa ulioje wa madhambi juu ya washirikina kwa utawala wa Ally, kwa kile unachowalingania ewe Muhammad, kutokana na utawala wa Ally

Hivi ndivyo ilivyoandikwa kwenye asili ya kitabu[3]. Na kutoka kwa Abi Abdillah amesema:

(سَأَلَ سَائِل بعذاب واقع للكافرين بولاية عَلِيٍّ ليس له دافع)

Ameuliza muulizaji kwa adhabu iliyothibiti, kwa mwenye kukufuru utawala wa Ally hakuna kwake yeye mtetezi.

---

[1] Angalia kitabu: Sharhu Usuulil Kaafi: (J. 7, Uk. 66).

[2] Angalia kitabu: Sharhu Usuulil Kaafi: (J. 7, Uk. 66).

[3] Angalia kitabu: Sharhu Usuulil Kaafi: (J. 5, Uk. 301).

kisha akasema: Wallahi hivi ndivyo Jibril (عليه السلام) alivyoteremka nayo kwa Muhammad ﷺ[1]

62- Mashia wanatumia hadithi ya Thaqalayn kuwa ndio hoja juu ya kuwepo kwa Maimamu wao. kuna Thiqlul Akbar ambayo ni Qur'an na Thiqlul Asghar ambayo ni Maimamu, na asiye wakubali Maimamu kama wanavyo itakidi Mashia ithnaasharia, basi huyo ni kafiri ametoka katika uislamu, kwa sababu anatia dosari katika uimamu na kukingwa kwao na kutenda dhambi, Ama mwenye kuitia ila Thiqlul Akbar ambayo ni Qur'ani huyo ni mujtahid, hata akikosea hulipwa, na kwa hivyo hata maulamaa wao wanapoulizwa kuhusiana na (Annuur-Atwabrasiy katika kitabu chake Faslul-khitwaabi fii bayaani tahriifi kitaabi rabbil arbaab), wanasema Huyo ni mwanazuoni mheshimiwa, amejitahidi akakosea, atapata ujira mmoja!!!

63- Lau kama mtu anataka kuingia katika Ushia, je afuate madhehebu gani miongoni mwa madhehebu mbali mbali ya kishia?! Kati ya Ithnaasharia, Ismailiyyah, Annuswairiyya, Zaidiyya, na Duruuzi....., na wote hao wanadai kujinasibisha na Ahlul Bait, wanakiri uimamu, na kuwafanyia uadui Mas-

[1] Angalia kitabu: Usuulul Kaafi: (J. 1, Uk. 422).

wahaba?! Na wote wanaitakidi uimamu wa Ally bin Abi Twaalib ﷺ na kwamba uimamu ni nguzo, na yeye ndiye khalifa baada kufa Mtume ﷺ tu, na wao ndio wenye asili ya dini..!

64- Ikiwa Mashia wanapokea elimu yao kutoka katika chanzo kimoja, kwa nini kuna tofauti kubwa katika hadithi zao? Anasema sheikh wa kishia Abu Jafar Muhammad ibn Al Hassan Attwuusiy katika mwanzo wa kitabu chake (Tahdhiib al Ahkaami[1] moja ya vitabu vyao vinne: "Kila sifa njema zinamstahikia Allah, mtawalia wa haki na mwenye kuistahiki na swala zake ziwe juu ya mbora wa viumbe wake Muhammad ﷺ, wamenielezea baadhi ya marafiki zangu katika Shia wetu kuhusu hadithi za wataalamu wetu Allah awape nguvu na awarehemu waliotangulia miongoni mwao, na tafauti kubwa inayoonekana kiasi ambacho hakuna hadithi inayotajwa ila itakuja nyengine inayo pingana nayo, na hakuna hadithi iliyosalimika, jambo ambalo limewapa nafasi kubwa wapinzani wetu kuyaponda madhebu yetu.

Na anasema Mshia (Raafidhwah) Sayid Daldaari Ally Al Lak-hanawii katika kitabu cha (Asasul Usuul):

---

[1] Angalia kitabu: Tahdhiibul Ahkaam: (J. 1, Uk. 1).

"Hakika hadithi zinazo pokewa kutoka kwa maimamu zimetafautiana sana, hupati hadithi isipokuwa kuna nyingine inayopingana nayo, wala hakuna riwaya inayokubaliana na mwenziwe, jambo ambalo limewafanya baadhi ya watu kutoka katika Ushia.... [1]".

Na anasema mwanazuoni wao, Mhakiki, Mwenye hikima, Mpekuzi na sheikhe wa kishia Husein bin Shihaabi Ddiin Al-karkiy katika kitabu chake (Hidaayatul abraari ilaa twariiqil aimmatul at-haar): "Hilo ndio lengo ambalo amelitaja mwanzo wa kitabu chake Attah-dhiib ya kwamba ametunga kitabu hichi ili kuondoa mgongano uliopo baina riwaya zetu, baada ya kusikia kwamba baadhi ya Mashia wametoka katika madhehebu kwa sababu hiyo.

Hivi ndivyo maulama wa Shia Ithnaasharia wanavyokubali kuwepo mgongano katika madhehebu yao, na Allah anasema:

﴿وَلَوْ كَانَ مِنْ عِندِ غَيْرِ ٱللَّهِ لَوَجَدُواْ فِيهِ ٱخْتِلَٰفًا كَثِيرًا﴾

"Lau kuwa ingetoka kwa asiye kuwa Allah, bila shaka wengekuta ndani yake khitilafu nyingi[2].

65- Baadhi ya Mashia wanajiita majina ndani yake

---

[1] Chapa ya Al Lak-hanawi India.

[2] Surat An Nisaa/82.

kuna kumuabudu asiyekuwa Alla, mfano: (Abdul Husein, Abdul Aimmat, Abdu Rridhwaa, na mengineyo), je wameyatoa wapi majina kama haya? Je kuna dalili juu ya kufaa kujiita (mja wa Fulani) isiyokuwa mja wa Allah mtukufu? na je kuna yeyote miongoni mwa (maimamu) amejiita yeye au mtoto wake kwa majina kama haya?

66- Turba ya Hussein ina utukufu mkubwa kwa mashia, je udongo huu ulikuwepo na ukawa na utukufu katika zama za maimamu wa Ahlul Bait.

67- Mashia wanaabudu kwa kujipiga makofi usoni na mwilini na kulia kwa kumuombolezea Husseini رضي الله عنه na Ahlu Bait wake, wakati kuna vitabu vya kishia ambavyo vinakataza mambo hayo.

Katika tafsiri ya Asswaafii katika kutafsiri aya Allah:

﴿وَلَا يَعْصِينَكَ فِي مَعْرُوفٍ﴾

"Wala hawatakuasi katika jambo jema[1]"

"Msijipige makofi, wala msizichune nyuso, wala msinyofoe nywele, wala msichane nguo, **wala msitie weusi nguo (msivae nguo nyeusi),** wala msijiapize, Mtume ﷺ akapokea ahadi yao (baia) juu ya hayo".

[1] Surat Al Mumtahina/12.

Na Mtume ﷺ amesema: **"Kuomboleza na kulia kwa makelele ni** katika mambo kijahiliya [1]".

Na Ally رضي الله عنه amesema baada kufa Mtume ﷺ akimwambia: "Lau kama hukukataza masikitiko, na ukaamrisha subra basi tunge yamaliza (kwa kukumwagia) maji ya mito [2]".

Na imepokewa kutoka kwa Ally رضي الله عنه amesema: "Mwenye kujipiga mkono wake pajani pake wakati wa msiba amali zake zimeporomoka [3]".

Katika hali hii hawaoni mashia kuwa wanakwenda kinyume na kile alichoamrisha Allah na Mtume ﷺ na Maimamu pia.

Ikiwa kujipiga makofi kwa ajili ya msiba ni katika matendo yaliyo ruhusiwa na sheria si angekuwa anaestahiki zaidi kufanyiwa ni Mtume ﷺ na mwanawe mtoharifu Bi Fatma, je Ally رضي الله عنه na jamaa zake waliwafanyia hivyo?

68- Mashia wanaabudu kwa kuvaa nguo nyeusi kama ishara ya huzuni yao juu ya Huseini رضي الله عنه, wakati

---

1 Angalia kitabu: Man laa yahdhuruhul Faqiih: (J. 4, Uk. 271-272).

2 Angalia kitabu: Nahjul Balaagha: (Uk. 576). Na Mustadrakul Wasaail: (J. 2, Uk. 445)

3 Angalia kitabu: Al Khiswaal: (Uk. 621), na Wasaailu Sshiia: (J. 3, Uk. 270).

riwaya za Ahlil Bait zinakataza kwa uwazi kuvaa nguo nyeusi. Miongoni mwa hizo: Imepokewa kutoka kwa Ally رضي الله عنه amesema: **"Msivae nguo nyeusi kwani hilo ni vazi la Firauni)**[1] na imekuja katika tafsiri As Swaafii katika kutafsiri aya:

﴿وَلَا يَعْصِينَكَ فِي مَعْرُوفٍ﴾

(Wala hawatakuasi katika jambo jema[2]

kwamba Mtume ﷺ alichukua ahadi kutoka kwa wanawake juu ya kwamba **wasivae nguo nyeusi,** (kwa ajili ya msiba) wala wasichane nguo wala wasiombe maangamizo [3].

69- Wanazuoni wa Kishia wanaona kwamba viungo vya kusujudiu katika swala ni vinane (paji la uso, pua, viganja vya mikono, magoti na miguu (ncha za vidole vya miguu), viungo hivi ni wajibu viguse ardhi wakati wa kusujudu [4].

Kisha wanasema ni wajibu kusujudu juu ya kitu

---

1 Angalia kitabu: Man laa yahdhuruhul Faqiih: (J. 1, Uk. 232) cha Ibn Baabawayhi Al Qummi, na pia ameipokea Al Hurrul Aamiliy katika Wasaailu Sshiia: (J 2, Uk. 916).

2 Surat Al Mumtahina/12.

3 Angalia Tafsiru Sswaafi: (J. 5, Uk. 166).

4 Angalia kitabu: Wasaailu Sshiia: (J. 3, Uk. 598) cha Al Hurrul Aamiliy.

kisicho liwa wala kuvaliwa, ndio maana wanaweka udongo chini ya mapaji ya nyuso zao[1], lakini hawaweki udongo chini ya kila kiungo katika viungo vya kusujudia?!

Haya ndiyo yaliyo wezekana kuyaandika, na tunamuomba Allah atupe Ikhlaas katika maneno na matendo yetu, na atuongoze katika njia yake iliyonyooka.

Swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad na Jamaa zake na Maswahaba zake.

وصلى الله على سيدنا محمد وعلى
آله وصحبه وسلم تسليماً كثيراً

[1] Angalia kitabu: Al Jaamiu Lis Sharaai': (Uk. 70) Al Hilliy.